**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA WAZIRI MKUU KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

Ofisi ya Bunge,
S. L. P 941,
**DODOMA**

Mei, 2015.

## YALIYOMO

1.0 UTANGULIZI ........................................................................................ 2

2.0 YALIYOBAINIKA KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO 3

3.0 UZINGATIAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 ........................................................................ 6

4.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015............................................................................................ 8

5.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 ............................................................ 9

4.1 Makadirio ya Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ........... 9

4.2 Makadirio ya Matumizi ya kawaida ................................................ 10

5.1 Waziri Mkuu na Ofisi ya Waziri Mkuu: Fungu 25 Na 37 .................. 10

5.2 Msajili wa Vyamavya Siasa: Fungu 27 ............................................ 16

5.3 Mfuko wa Bunge: Fungu 42.............................................................. 18

5.4 Tume ya Taifa ya Uchaguzi: Fungu 61............................................ 20

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA WAZIRI MKUU KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016**

---

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni za 99 (5) na (9) na 114 (11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili 2013, naomba kuwasilisha katika Bunge lako tukufu Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu yaliyo chini ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera,Uratibu na Bunge inajumuisha Mafungu matano yafuatayo:-

i) Fungu 25 – Waziri Mkuu;

ii) Fungu 27 – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa;

iii) Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu;

iv) Fungu 42 – Mfuko wa Bunge; na

v) Fungu 61 – Tume ya Taifa ya Uchaguzi.


**Mheshimiwa Spika,** Katika Taarifa hii, Kamati inaripoti kuhusu yaliyobainika katika Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Uchambuzi wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kutokana na uchambuzi huo.

## 2.0 YALIYOBAINIKA KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

**Mheshimiwa Spika**, ili kujiridhisha na mwenendo wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, Taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati tarehe 05 Mei, 2015 inaonesha kuwa hadi tarehe 31 Machi, 2015, Ofisi ya Waziri Mkuu – Fungu 37, Ofisi ya Bunge Fungu 42 na Tume ya Taifa ya Uchaguzi – Fungu 61 kwa pamoja zilikuwa zimepokea **shilingi 21,777,497,450**/= Kiasi hicho ni sawa na asilimia 75.7 ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Miradi hiyo.


Aidha, Wakati wa kupitisha Bajeti za Mafungu hayo, uwiano wa Bajeti zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya Maendeleo kwa kila Fungu ikilinganishwa na Jumla ya fedha za Miradi ya Maendeleo kwa mafungu hayo matatu ni kuwa Bajeti ya Ofisi ya Bunge kwa miradi ya Maendeleo ni asilimia 30.4 ya Fedha zote za Miradi ya Maendeleo kwa taasisi hizo tatu, Waziri Mkuu asilimia 62.8 na Tume ya Taifa ya Uchaguzi asilimia 6.8 kama inavyoonekana katika Chati 01 ya Taarifa hii.

**Chati 01:** Mchanganuo wa Uwiano wa Bajeti zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo




**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo uwiano wa upatikanaji wa fedha kwa taasisi hizo tatu ikilinganishwa na jumla ya fedha zote zilizopatikana kwa ajili ya miradi ya Taasisi hizo ulibadilika. Uchambuzi wa Kamati umeonesha kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu imepanda kufikia asilimia 82.1 ya Fedha zilizopokelewa, Ofisi ya Bunge imeshuka kufikia asilimia 17.2 ya fedha zilizopokelewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeshuka zaidi kufikia asilimia 0.7 ya jumla ya fedha zilizopokelewa. Mchanganuo huo unaonekana katika Chati 02 ya Taarifa hii.

**Chati 02:** Mchanganuo wa Uwiano wa Upatikanaji wa fedha




**Mheshimiwa Spika,** Mwenendo huo wa upatikanaji wa fedha umekuwa mzuri kwa miradi ya Maendeleo chini ya Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu na si mzuri kwa Fungu 61- Tume ya Taifa ya Uchaguzi yenye jukumu muhimu na zito kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 na pia 2015/2016. Wakati Ofisi ya Waziri Mkuu ilipata asilimia 99 ya bajeti yake iliyoidhinishwa kwa miradi ya maendeleo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilipata asilimia 7.4 ya bajeti yake iliyoidhinishwa kwa miradi ya Maendeleo. Aidha, Ofisi ya Bunge iliyotarajiwa kuendelea na zoezi la Ujenzi wa Ofisi za Wabunge ilipata asilimia 42. 9 ya bajeti yake ya maendeleo, kiasi ambacho ni pungufu ya nusu ya Bajeti iliyoidhinishiwa kwa ajii hiyo.

## 3.0 UZINGATIAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

**Mheshimiwa Spika,** Wakati wa Kupitia na Kuidhinisha Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini ya Ofisi hii, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika jumla ya mambo thelathini (30) kwa Mafungu matano chini ya Ofisi hii. Ili kujiridhisha na namna Serikali ilivyozingatia maoni na kutekeleza ushauri wake, Kamati ilipokea Taarifa ya uzingatiaji wa maoni na Utekelezaji wa ushauri uliotolewa. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, taarifa hiyo inaonyesha kwamba yapo mambo yaliyozingatiwa na mengine hayakuzingatiwa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa mambo yaliyoshauriwa ni thelathini, naomba kutaja mifano michache ya Ushauri uliozingatiwa na hata ule ambao haujazingatiwa ili kuliwezesha Bunge lako tukufu kufuatilia kwa karibu zaidi na kutekeleza wajibu wake ipasavyo katika kuisimamia Serikali. Mfano wa Ushauri uliotekelezwa na kuzingatiwa ni kuhusu Ofisi ya Bunge. Kamati ilishauri kuwa Ofisi hii imuelekeze Mtoa huduma ya Matibabu kwa Wabunge (Jubilee Insurance) kutoa elimu kwa Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na utaratibu wa kutoa huduma hiyo na aina ya Hospitali zinazohusika na mkataba baina ya Ofisi hii na Kampuni hiyo ya Bima.

Taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati zinaonesha kuwa Kamati zote za Bunge zilifanyiwa Semina iliyoendeshwa na Jubilee Insurance. Katika Semina hiyo, Waheshimiwa Wabunge walieleweshwa kuhusu taratibu za utoaji wa huduma na Hospitali zinazohusika.

**Mheshimiwa Spika**, Mfano mwingine wa Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati ambao Serikali imeuzingatia,unahusu Serikali kuiwezesha Tume ya Taifa kifedha na imeweza kuwapeleka Watumishi wengi zaidi kushuhudia chaguzi mbalimbali zinazofanyika nchi jirani kwa lengo la kujifunza namna bora ya kusimamia uchaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kutekeleza baadhi ya maoni na ushauri wa Kamati, kuna sehemu kubwa ya ushauri haijazingatiwa. Kwa mfano, ushauri kuhusu kupunguza tozo la mapato ya Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali yanayotokana na shughuli za upigaji chapa haujazingatiwa. Maelezo ya Serikali yanaonesha kuwa hadi sasa bado Serikali haijafanyia kazi ushauri huo.

**Mheshimiwa Spika**, Mfano mwingine wa kutokutekelezwa kwa ushauri wa Kamati ni kuhusu fedha za kuiwezesha Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuanza mchakato wa ujenzi wa jengo la Ofisi. Taarifa inaonesha kuwa Serikali haijazingatia hilo kwa hoja kuwa rasilimali nyingi zimeelekezwa kwenye uboreshaji wa

daftari la Kudumu la Mpiga Kura , Kura ya Maoni na Uchaguzi Mkuu.Ni maoni ya Kamati kuwa jukumu hilo la Tume halikupaswa kufuta umuhimu wa kuiongezea Tume fedha kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi.

## 4.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu namna bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Uratibu na Bunge na taasisi zake ilivyotekelezwa na hivyo kupitia taarifa iliyowasilishwa kwa ajili ya uchambuzi. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa utekelezaji wa malengo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ulikabiliwa na changamoto mbalimbali kama zilivyoripotiwa na Waziri wa nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge. Miongoni mwa changamoto hizo ni:-

i) Wizara na Taasisi nyingi za Serikali ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, Ofisi ya Bunge na Taasisi zilizochini ya Waziri Mkuu kuchelewa kupata fedha katika mwaka wa fedha 2014/2015. Hali hii imeripotiwa kusababisha baadhi ya shughuli zilizopangwa kutotekelezwa kabisa na nyingine kutokutekelezwa kwa wakati.

ii) Wakati Bunge likitekeleza majukumu yake ya kikatiba, imekuwa ikitokea umuhimu wa kuundwa kwa Kamati Maalumu au Teule za Bunge ambazo gharama zake

hazikuwepo katika makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha husika. Hali hii inaathiri mwenendo wa matumizi ya fedha za mfuko wa Bunge ikilinganishwa na mahitaji halisi ya matumizi yaliyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto hizo zinahitaji kufanyiwa kazi ipasavyo badala ya kuishia kuziorodhesha. Kwa mfano, suala la Kujitokeza kwa umuhimu wa kuundwa kwa Kamati maalum za Bunge haliepukiki na ni utaratibu unaoliwezesha Bunge kutekeleza vema majukumu yake. Kwa sababu hiyo, ni maoni ya Kamati kuwa si utaratibu mzuri inapotokea hali hiyo kutoongeza fedha katika Fungu 42 kwa madhumuni hayo.

## 5.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

### 4.1 Makadirio ya Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2015/2016

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati kuhusu Makadirio ya matumizi unaonesha kuwa kuna ongezeko dogo sana la makadirio ya maduhuli ikilinganishwa na makadrio ya mwaka wa fedha 2014/2015. Wakati mwaka wa fedha 2014/2015 Makadirio yalikuwa ni jumla ya Shilingi **4,998,233,000/-** Makadirio ya maduhuli kwa mwaka wafedha 2015/2016 ni Sh. 5,009,930,000/-. Ongezeko hilo ni dogo sana ukilinganisha na uwezo wa Taasisi hizo wa kukusanya maduhuli , Ofisi ya Bunge na Msajili wa vyama vya siasa wamekadiriwa kukusanya kiasi

kilekile cha mwaka wa fedha 2014/2015. Ni dhahiri kuwa hakuna vyanzo vipya katika Mafungu ya Taasisi hizo.

## 4.2 Makadirio ya Matumizi ya kawaida

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi unaonesha kuwa kuna ongezeko la asilimia 111.7 ikilinganishwa na Makadiro ya Matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 204/2015. Kwa upande wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kuna ongezeko la asilimia 79.7 ikilinganishwa na bajeti ya miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Kamati ina maoni kuwa ongezeko hilo halitakuwa na maana yoyote iwapo upatikanaji wa fedha hautakuwa na uhakika. Ni vema Serikali ikaweka mikakati ya kuwezesha upatikanaji wa fedha kadiri ya bajeti inayoidhinishwa na Bunge.

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia taarifa iliiyowasilishwa mbele ya Kamati mnamo Tarehe 5 Mei 2015, pamoja na maombi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 kama yalivyoainishwa kwa kila fungu, Kamati inatoa maoni na mapendekezo kama ifuatavyo:

## 5.1 Waziri Mkuu na Ofisi ya Waziri Mkuu: Fungu 25 Na 37

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kupitia malengo ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambaye ndiye msaidizi Mkuu wa Rais, Mratibu na Msimamizi Mkuu wa shughuli na mipango yote ya Serikali katika sekta zote nchini na ndani ya Bunge, mhimizaji mkuu wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya wananchi mijini na vijijini na kuhakikisha kuwa kuna utendaji na usimamizi mzuri wa Serikali unaozingatia misingi ya utawala bora ili kuleta maendeleo endelevu, Kamati inashauri yafuatayo:-

i) Ofisi hii iimarishwe kikamilifu kwa kutengewa fedha za kutosha na Rasilimali watu na vitendea kazi vya kisasa ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa lengo la kuwezesha uchaguzi kuwa haki, amani na utulivu. Aidha, fedha zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 kuhusiana na Maandalizi ya Uchaguzi Mkuu zitolewe zote kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ili kuhakikisha kuwa Maandalizi hayo yanafanyika kama yalivyopangwa.

ii) Ofisi ya Waziri Mkuu iweke utaratibu endelevu wa kutatua changamoto zinazokabili sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii mapema iwezekanavyo ili kuepusha migomo isiyo ya lazima ya wafanya biashara na kunusuru athari za kiuchumi na kijamii kwa lengo la kuimarisha uchumi, amani na utulivu.

iii) Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe inaandaa Kanuni za Uchaguzi mapema na kuzisambaza kwa wadau sanjari na kuongeza kasi ya utoaji elimu ya mpigakura kwa wananchi ili wadau wote wa uchaguzi washiriki uchaguzi huo wakiwa na taarifa na elimu sahihi kuhusu masuala ya uchaguzi na kanuni za kufuata katika uchaguzi huo.

iv) Ofisi ya Waziri Mkuu ifanye tathmini ya athari kubwa zilizotokana na ukame ulioyakumba baadhi ya maeneo pamoja na mvua zinazoendelea katika maeneo mbalimbali nchini ili kuweza kubaini hasara na ukubwa na maafa hayo na hatimaye kuchukua hatua za haraka za kurejesha Miondombinu iliyoharibika katika hali yake awali.

Aidha, kwa maeneo ambayo tathmini imefanyika na athari mbalimbali kubainika kisha Mheshimiwa Waziri Mkuu kutoa ahadi ya kuchukua hatua stahiki, Serikali itekeleze ahadi zote zinazotolewa katika maeneo hayo.

v) Kuhusu mradi wa kuendeleza eneo la Makaburi ya Viongozi Mkoani Dodoma, Kamati inaendelea kushauri Serikali itilie maanani uwepo wa mradi huu kwa kuendelea kuutengea fedha na kuhakikisha kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya Mradi huu zinatolewa ili zifanye kazi inayokusudiwa.

vi) Serikali ikamilishe awamu ya kwanza ya ujenzi na kuanza awamu ya pili inayohusisha ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Waziri Mkuu Dodoma ili kufanikisha azma njema ya Serikali katika ujenzi huo. Aidha, Serikali ihakikishe kuwa kasi ya utoaji wa Fedha zinazotengwa kwa ajili ya ujenzi huo inaongezwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa fedha zilizotengwa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 zinatolewa kabla ya kuisha kwa mwaka wa fedha.

vii) Ili kutimiza azma ya Serikali ya kuhamishia Makao Makuu ya Nchi, Dodoma:-

a) Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kuendeleza na kupanga miji ikiwemo makao Makuu ya Serikali Dodoma. Elimu ikitolewa ipasavyo itawawezesha wananchi kujiepusha na uvamizi wa maeneo ya mji au ujenzi holela ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima kati ya Mamlaka na wananchi.

b) Ili kutimiza azma ya serikali kuamua kuhamishia Makao Makuu ya Nchi Dodoma tangu mwaka 1973, Serikali iweke kipaumbele kwa kutenga bajeti ya kutosha na kuhakikisha fedha zinazotengwa kwa ajili ya kuendeleza mji zinatolewa ikiwa ni pamoja na kiasi cha Shilingi 500,000,000/= zilizotengwa kwa Mwaka

2014/2015 kwa ajili ya kuendeleza makao makuu Dodoma.

c) Kwa kuwa azma ya Serikali ya kuendeleza Makao Makuu Dodoma ilitangazwa kwa amri, ni muda muafaka sasa kwa Serikali kuleta Muswada wa Sheria mahsusi kuhusu uanzishwaji na usimamizi wa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma.

viii) Kwa kuwa Idara ya maafa ilianzishwa kwa nia ya kuweka mfumo madhubuti wa kukabiliana, kutekeleza na kuratibu kikamilifu shughuli za kubiliana na maafa:-

a) Serikali iharakishe Kanuni za Sheria ya Usimamizi wa Maafa ili kuwezesha utekelezaji wa Sheria hiyo na kuhakikisha kuwa Sheria hiyo inaanza kutumika mapema iwezekanavyo. Kuanza kutumika kwa kanuni na Sheria ya Usimamizi wa Maafa kutawezesha nchi yetu kukabiliana kikamilifu na maafa ya aina mbalimbali na kuwaepusha na athari kubwa zinazotokana na maafa.

b) Mara baada ya Sheria Mpya ya Maafa itakapoanza kutumika, taasisi zinazoanzishwa kwa Mujibu wa Sheria hiyo ziboreshwe kwa kujengewa uwezo wa fedha na rasilimali watu, ujuzi na vifaa, kwa lengo la kuisaidia nchi yetu kukabiliana na maafa ya aina mbalimbali yatakayoweza kujitokeza kama ilivyokusudiwa.

c) Katika kipindi cha mpito kabla Sheria Mpya haijaanza kutumika, Serikali iharakishe kutoa huduma zinazostahili kama chakula na madawa kwa wahanga wa maafa ili kupunguza athari kubwa zaidi zinazoweza kujitokeza kama hatua za haraka hazitachukuliwa.

ix) Serikali iboreshe Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kununua Mashine zinazoweza kuchapa pande mbili za karatasi kwa wakati mmoja na kwa haraka. Aidha Mtambo Mmoja Mkubwa wa umaliziaji (print-finishing) ili kuwezesha kukusanya na kufunga vitabu na majarida mbalimbali yanayochapishwa kwa haraka na ufanisi.

x) Serikali iharakishe mchakato wa kumtafuta Mataalam Mshauri Muelekezi ambaye atafanya utafiti wa namna bora ya kuendesha idara hii kwa kushirikana na wabia wengine ili kujiendesha kibiashara na kujitegemea.

xi) Serikali ihakikishe fedha zinazotengwa kwa ajili ya idara hii,zinatolewa zote na kwa wakati ili kuiwezesha ofisi hii kufufuliwa na kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa dhumuni la kuanzishwa kwake.

xii) Pamoja na Serikali kuwa na mfumo wa utekelezaji wa ahadi zinazotolewa na viongozi wakuu wa Nchi wakiwemo Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu, hata

hivyo utekelezaji wa ahadi hizo umekuwa si wa kiwango cha kuridhisha kwa kuwa taarifa kuhusu ahadi hizo kutoka Mikoani na Wilayani huchukua mda mrefu kuzifikia mamlaka za utekelezaji, ili kuhakikisha kuwa ahadi hizo zinatekelezwa, Kamati inashauri Serikali iandae utaratibu mwingine madhubuti wa kuratibu utekelezaji wa ahadi hizo ikiwepo kuanzisha idara maalumu katika Ofisi ya Waziri Mkuu itakayokuwa inashughulikia kwa karibu nakuratibu utekelezaji wa ahadi za viongozi hao.

xiii) Katika kuelekea uchaguzi Mkuu wa Mwezi Oktoba, 2015, Ofisi ya Waziri Mkuu katika kusimamia na kuratibu shughuli za Serikali, ihakikishe inatoa elimu kikamilifu kwa wananchi kuhusu umuhimu na jukumu la kila mwananchi la kulinda na kudumisha amani na utulivu nchi yetu pasipokujali tofauti za dini, itikadi na tofauti za vyama.

## 5.2 Msajili wa Vyama vya Siasa: Fungu 27

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa ni idara ya Serikali inayojitegemea iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Vyama vya Siasa Na.5 ya mwaka 1992. Idara hii ilianzishwa kwa madhumuni mahsusi ya kufanikisha mfumo wa Demokrasia nchini ulioanzishwa baada ya marekebisho ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo mfumo wa Vyama vingi ulianzishwa. Ofisi hii ni muhimu kwa ustawi na

ushamiri wa demokrasia hapa nchini. Ili kuhakikisha kuwa demokrasia inaendelezwa na kuiimarishwa kikamilifu, Kamati inashauri Kama ifuatavyo:-

i) Kwa kuwa shughuli za siasa zinaongezeka siku hadi siku, Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa iwezeshwe kikamilifu kwa kutengewa bajeti ya kutosha na kuajiri rasilimali watu wa kutosha na wenye weledi unaostahili pamoja na nyenzo za kisasa ili iweze kukabiliana na kasi ya ongezeko la shughuli za siasa pamoja na kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa lengo la kukuza democrasia kwa ustawi wa Taifa letu.

ii) Kwa kuzingatia kuwa nchi yetu inaelekea katika uchaguzi mkuu, serikali iharakishe mchakato wa kuleta Bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa- "The political parties Act, CAP 258 R.E 2002" pamoja na Sheria ya gharama za Uchaguzi ya Mwaka 2010 ili kuondoa dosari zilizopo katika sheria hizo kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba 2015.

iii) Kwa kuwa Ofisi ya Msajili wa vyama vya siasa ni taswira ya nchi katika kuendeleza na kukuza Demokrasia nchini, Serikali ihakikishe inajenga majengo ya kisasa kwa ajili ya Ofisi hii ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kulinda hadhi na heshima ya nchi yetu.

iv) Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa iendelee kuratibu kwa karibu zaidi masuala ya maridhiano kwa Vyama vya Siasa

kupitia Baraza la demokrasia nchini( Tanzania Centre for Democracy) ili kukuza na kuimarisha Demokrasia Kwa lengo la kudumisha amani na utulivu nchini.

v) Ofisi ya Msajili wa Vyama vya siasa iendelee kufuatilia kuratibu uchukuaji wa hatua stahiki kwa vyama vya siasa vinavyokiuka sheria na taratibu za uendeshaji wa shughuli za siasa.

vi) Msajili wa vyama vya siasa nchini kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Uchaguzi watoe elimu ya kuhusu sheria ya Gharama za Uchaguzi(The Election Expenses Act) na Sheria ya Taifa ya Uchaguzi(The National Election Act) kwa wadau wote wa uchaguzi kabla ya wakati wa Uchaguzi ili kuwawezesha kuelewa matakwa ya sheria hizo na kuyazingatia wakati wa Uchaguzi Mkuu.

## 5.3 Mfuko wa Bunge: Fungu 42

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Ofisi ya Mheshimiwa Spika pamoja na Tume ya Utumishi wa Bunge kwa kuendelea kutoa **ushauri na mapendekezo kwa Mheshimiwa Rais ya kuboresha maslahi ya Waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Bunge** ili kuhakikisha kuwa Wabunge na watumishi wa Bunge wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kuleta tija kwa taifa. Hata hivyo ili kuhakikisha Bunge linatekeleza majukumu yake ipasavyo Kamati inashauri yafuatayo:

i) Ofisi ya Bunge ifuatilie kwa karibu Mchakato wa makabidhiano ya Ofisi 75 zilizojengwa na TAMISEMI kwa ajili Wabunge katika Majimbo husika na kuziwekea samani ili kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kuanza kuzitumia katika kuwahudumia wananchi kwa karibu na kwa ufanisi zaidi.

ii) Serikali ifuatilie na kumaliza mgogoro wa kuhusu umiliki wa kiwanja kilichopo nyuma ya Ofisi ndogo za Bunge Dar es salaam ili Mkataba baina ya Ofisi ya Bunge na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) wa kujenga jengo la Ofisi katika eneo hili uweze kuetekelezwa na kukamilishwa mapema iwezekanavyo.

iii) Ofisi ya Bunge iendelee kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ili kuweka vigezo sahihi vya kuyatambua na kutenga maeneo ya ujenzi wa Ofisi za Waheshimiwa Wabunge. Lengo ni kuhakikisha kuwa Ofisi hizo zinajengwa katika maeneo stahiki kwa maslahi ya wananchi ili ziweze kutumika kwa miaka mingi inayokuja.

iv) Ofisi ya Bunge iiwezeshe kikamilifu Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ili iweze kufutilia kwa karibu mchakato wa maandalizi ya Uchaguzi Mkuu ikiwemo uandikishaji wa Daftari la Mpiga Kura unaoendelea katika maeneo mbalimbali nchini kwa lengo la kuhakikisha kuwa zoezi linaendeshwa kwa ufanisi.

v) Ofisi ya Bunge iharakishe mchakato wa kutafuta ofisi kwa ajili ya waheshimiwa wabunge wawapo Dodoma ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa umakini na Ufanisi zaidi. Aidha Kamati inashauri kuwa Ofisi ya Bunge ianze kufikiria uwezekano wa kujenga BUNGE TOWER badala ya kupanga ofisi kwa ajili ya Wabunge ili kuepusha gharama kubwa za kulipia pango.

vi) Tume ya Utumishi wa Bunge iendelee kusimamia na kutetea maslahi ya Wabunge na Watumishi wa Bunge na hasa kuwapandisha vyeo Watumishi wa Bunge wanaostahili kupandishwa vyeo ili kuwaepusha watumishi hao kukaa muda mrefu katika cheo kimoja.

vii) Serikali iiwezeshe Ofisi ya Bunge kwa kuitengea bajeti ya kutosha kwa ajili ya kujenga kijiji cha Bunge katika eneo la Itega lililopo manispaa ya Dodoma ili kuwawezesha Waheshimiwa wabunge kuwa na makazi ya uhakika na usalama wawapo Dodoma kwa lengo la kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

### 5.4 Tume ya Taifa ya Uchaguzi: Fungu 61

**Mheshimiwa Spika ,**Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeundwa kwa mujibu wa Ibara ya 74 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Tume hii kwa mujibu wa Katiba na Sheria ya Taifa ya Uchaguzi (The National Election Act) imepewa jukumu la kusimamia na kuratibu uendeshaji wa

Uchaguzi wa Rais na Wabunge katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia kuratibu na kuendesha uchaguzi wa madiwani kwa Tanzania Bara . Kamati inatambua jitihada za Serikali katika kuiwezesha Tume hii ili iweze kutekeleza wajibu wake wa Kikatiba wa kusimamia uchaguzi hapa nchini, Hata hivyo ili kuboresha na kuimarisha Taasisi hii muhimu Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

i) Ili Tume hii iweze kutekeleza uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Mpiga Kura ni vyema Serikali ikaongeza kasi ya utoaji wa fedha zinazotengwa kwa ajili ya kazi hiyo muhimu.

ii) Serikali iongeze msukumo wa kuingiza mashine za BVR zinazotumika katika zoezi la kuandikisha wapiga Kura zilizosalia ambazo ni 3140 kati ya mashine 8000 zilizoagizwa na kuzilipia ili kuiwezesha Tume kukamilisha zoezi la Uandikishaji mapema iwezekanavyo.

iii) Tume ya Taifa ya Uchaguzi iharakishe kukamilisha zoezi la uandikishaji wa Daftari la Kudumu la Mpiga Kura kwa wananchi wote wenye sifa nchini ili kutoa nafasi ya kufanya uhakiki wa watu walioandikihwa kabla ya uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba, 2015.

iv) Tume kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iendelee kutoa elimu ya uraia na umuhimu wa kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Mpiga Kura na kupiga kura ili kuwahamasisha wananchi kujitokeza kupiga kura katika chaguzi mbalimbali Nchini na Kura ya Maoni.

v) Tume ya Taifa ya Uchaguzi iharakishe mchakato wa kugawa majimbo ambayo mipaka yake imebadilika kutokana na kuanzishwa kwa Mikoa, Wilaya na Halmashauri Mpya na hivyo kulazimika kubadilisha majina ya majimbo na kugawanya majimbo hayo.

vi) Tume ya Taifa ya Uchaguzi ihuishe kanuni za Uchaguzi mapema kwa kuwashirikisha wadau na kuhakikisha zinaeleweka vema kwa wananchi na wadau wote kabla hazijaanza kutumika ili kuwezesha kanuni hizo kuendana na wakati uliopo na kuhakikisha kuwa uchaguzi huo unafanyika kwa kufuata Sheria,Kanuni na Taratibu na kufanya uchaguzi kuwa huru,haki,utulivu na Amani.

vii) Serikali itenge fedha za kutosha na kutoa kwa wakati fedha zilizotengwa ili kuiwezesha Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuanza mchakato wa ujenzi wa Jengo la Ofisi yake ili kupunguza gharama za upangaji pamoja na kuiwezesha kufanya kazi katika mazingira bora na ya kisasa.

viii) Kwa kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatakiwa kuwa huru katika utekelezaji wa majukumu yake, Serikali iwezeshe Tume hii kuajiri watumisi wa kutosha watakaoweza kufanya kazi hadi katika ngazi ya mikoa na Halmashauri ili kuondoa dhana kwamba kwa kutumia watumishi wa Halmashauri katika chaguzi kunaifanya Tume kutokuwa huru.

ix) Kwa kuwa muda wa kuelekea uchaguzi umekaribia na bajeti kwa ajili hiyo inapitishwa hivi sasa, Serikali isimamishe zoezi la kugawa maeneo ya kiutawala ambayo hayatatengewa bajeti ili kuepusha adha ya kibajeti inayoweza kujitokeza.

## 7.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, napenda nitumie nafasi hii pia kukupongeza kwa dhati kwa jinsi unavyoliongoza Bunge hili ambalo ni chombo cha uwakilishi wa Wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali ili kuhakikisha kuwa ustawi wa wananchi ndio kipaumbele cha kwanza.

**Mheshimiwa Spika,** nimpongeze pia Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania, kwanza kwa jinsi anavyoratibu vizuri na kufuatilia kwa karibu shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Wizara zote katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwani sote tunatambua kuwa changamoto zinazoikabili Serikali yetu ni nyingi hivyo kuzisimamia shughuli zote hizo ni mzigo mkubwa.

Aidha, katika kipindi chote alichotumikia Nchi yetu Kama Waziri Mkuu umekuwa karibu sana na Ofisi ya Bunge na amekuwa tayari kuzishughulikia changamoto mbalimbali zikiwemo za Kamati za Bunge wakati zinapotekeleza majukumu yake kwa niaba ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** pia napenda nimshukuru Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama, (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge na , Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi, Idara na vitengo pamoja na Maafisa wote, kwa maelezo na ufafanuzi wa kina walioutoa kwa Kamati wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara hii na tayari kufanya kazi wakati wowote ambao Kamati ilihitaji kupata ufafanuzi kutoka kwao.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio haya. Umahiri na uzalendo wao kwa Nchi yetu uliwafanya kuvumilia na kufanya kazi hata katika mazingira magumu ili kukamilisha. Kwa heshima naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

1) Mhe. Jasson Samson Rweikiza, Mb - Mwenyekiti
2) Gosbert Begumisa Blandes, Mb -M/Mwenyekiti
3) Mhe. Abbas Zuberi Mtemvu, Mb - Mjumbe
4) Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mb - Mjumbe
5) Mhe. Nimrod Elirehema Mkono, Mb - Mjumbe
6) Mhe. Halima J. Mdee, Mb - Mjumbe
7) Mhe. Fakharia K. Shomar, Mb - Mjumbe
8) Mhe. Rukia Kassim Ahmed, Mb - Mjumbe
9) Mhe. Ali Khamis Seif, Mb - Mjumbe
10) Mhe. Felix Francis Mkosamali, Mb - Mjumbe
11) Mh, Abdallah Sharia Ameir, Mb - Mjumbe
12) Mhe. Mustapha B. Akunaay, Mb - Mjumbe
13) Mhe. Mariam Reuben Kasembe, Mb - Mjumbe
14) Mhe. Tundu A. Mughwai Lissu, Mb - Mjumbe
15) Mhe. Deogratias A. Ntukamazina, Mb - Mjumbe
16) Mhe. William Mganga Ngeleja, Mb - Mjumbe
17) Mhe.Nyambari C.M.Nyangwine.Mb - Mjumbe
18) Mhe. Ramadhan Haji Saleh - Mjumbe
19) Mhe. Zahra Ali Hamad, Mb - Mjumbe
20) Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Mjumbe

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa makini na madhubuti wa Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, nawashukuru ndugu

Charles Mloka, ndugu Matamus Fungo, Maria Mdulugu na Abdallah Selemani kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zake kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Jasson Samson Rweikiza, (Mb.)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA**
Mei, 2015